



KIBABII UNIVERSITY

UNIVERSITY EXAMINATIONS

2021/2022 ACADEMIC YEAR

SECOND YEAR FIRST SEMESTER

SPECIAL/SUPPLEMENTARY EXAMINATION

FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)

COURSE CODE: SWA 212/KIS 200

COURSE TITLE: NADHARIA ZA UHAKIKI WA FASIHI

DATE: 20/07/2022

TIME: 11:00AM-1:00PM

MAELEKEZO

Jibu maswali **matatu** pekee.

Swali la Kwanza ni la **lazima**

MUDA: Masaa Mawili (2)

KIBU observes **ZERO** tolerance to examinations cheating

Maswali

1. a) Bainisha sifa za urasimi kwa jumla. (alama 8)
b) Tofautisha kati ya uhakiki sadfa na uhakiki wa mapitio. (alama 4)
c) Eleza umuhimu wa uhakiki katika fasihi. (alama 8)
d) Dadavua sifa za nadharia mwafaka. (alama 10)
2. Onyesha uhalisia wa maisha kimaudhui kwa kurejelea riwaya ya kiu. Zingatia hoja zozote tano. (alama 20)
3. Kwa kurejelea nadharia ya umaksi, hakiki riwaya ya *Nyota ya Rehema*. (alama 20)
4. Pambanua namna uhalisiajabu unavyobainika katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*. (alama 20)
5. Hakiki shairi lifuatalo kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya umuundo. (alama 20)

KWA WALIMU WOTE

Sikilizeni wimbo huu:

Nilipokuwa mtoto niliitwa Chacha
Kwa matamshi yangu ya sasa
Nilipokuwa kijana niliitwa Chaupele
Nilipokuwa mtu mzima niliitwa Manywele
Nilipokuwa mwalimu nikaitwa Bure.

Huu utakuwa wimbo wako
Utakapostaafu urudipo nyumbani
Umelewa kangara na nyayo zako
Zikishindwa kulenga njia nyembamba vijijini.
Utakuwa kichekesho cha watoto
Watakaokuita, Ticha! popote upitapo.

Kumbuka mwalimu utakapostaafu.
Mijusi watataga mayai ndani ya viatu
Vyako vilivyokwisha visigino
Na ndani ya sidiria chakavu
Zilizoshikizwa kamba kwa kipini
Mende watazaliana ndani ya chupa tupu
Za marashi na za bia.

Na manyigu yatajenga ndani ya kofia
Zilizosahaulika kutani.
Utakapokufa nge watazaliana
Chini ya jiwe juu ya kaburi lako,
Na mlevi fulani akipita atapenga
Na kupangusa vidole kwenye jiwe pweke.
Mwanzo na mwisho wako ndio huo.

Lakini wakati ungali hai
Unaweza kubadilisha mkondo wa maji.
Lakini kwanza tuzungumze. Wewe na mimi.
Acha mioyo yetu izungumze.
Baada ya kunyanyaswa na kisha nusu mshahara,

Utafundisha tena nyimbo kuwasifu viongozi?
Utafundisha tena ngonjera?
Utapeleka tena wanafunzi asubuhi
Wakajipange barabarani kusubiri
Mgeni afikaye saa kumi, na apitapo
Apunga tu mkono kuwatia kichaa cha shangwe
Na huku nyuma mwasambaa na njaa?

Tazama hilo rundo la madaftari mezani
Utalimaliza kwa mshahara mkia wa mbuzi?
Tuzungumze. Nyinyi na mimi.
Acha mioyo yetu izungumze.
Mkiwa waoga na kujikunja kama jongoo
Mtawekwa kwenye vijiti na kutupwa
Nje ya ua, ndani mtawaacha
Wacheza ngoma wakitunga nyimbo mpya.

Sikilizeni walimu.
Anzeni kufundisha hesabu mpya:
Mjinga mmoja kujumlisha na wezi ishirini
Ni sawa na sufuri.
Fundisheni historia mpya:
Hapo zamani za sasa
Hapakuwa na serikali.

Sikilizeni kwa makini
Umoja hatuna:
Twasambaratika kama nyumbu.
Tulichonacho ni woga,
Na kinachotuangusha ni unafiki.
Lakini tusikate tamaa kama mbuni.
Tukiupata umoja bado tunayo silaha.
Kura.